

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

WIZARA YA FEDHA



BODI YA WATAALAM WA UNUNUZI NA UGAVI



TAARIFA KWA UMMA

USAJILI WA MITIHANI YA KATI YA PSPTB AWAMU PILI

(2ND MID SESSION EXAMINATIONS)

Dodoma 01 Julai, 2026.

Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi (PSPTB) inapenda kuwajulisha wadau wake kuwa, inatarajia kuendesha mitihani ya kitaaluma ya 2 ya PSPTB kuanzia tarehe **24/08/2026** hadi tarehe **28/08/2026**. Waombaji wenye sifa na nia ya kuomba kufanya mitihani hii wanaelekezwa kufanya usajili wa mitihani hii kupitia <https://registration.psptb.go.tz> na pia kuhudhuria madarasa ya mafunzo kama sehemu ya maandalizi ya mitihani hiyo. Mitihani hii itafanyikia katika kituo kimoja kilichoko **Dodoma** kama inavyooneshwa katika dirisha la usajili na mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 07/08/2026.

Waombaji wenye sifa ya kufanya mitihani ya kitaaluma ya agosti, 2026

- (a) Wahitimu wote waliomaliza Vyu vya Elimu ya Juu na Kati kwa ngazi za Shahada, Stashahada na Astashahada ya Ununuzi na Ugavi kwa kipindi cha kuanzia 2025 kurudi nyuma ambao hawakuwahi kufanya mitihani ya kitaaluma ya Bodi ya Wataalam wa Ununuzi na Ugavi.
- (b) Wafanyakazi wote wanaofanya kazi za Ununuzi na Ugavi katika sekta binafsi na umma pasipokuwa na cheti cha CPSP.
- (c) Wahitimu wenye taaluma nyingine nje ya ununuzi na ugavi kwa ngazi za stashahada shahada au wenye sifa za kitaaluma kutoka Bodi/Mabaraza ya taaluma husika na yanayotambulika na PSPTB.
- (d) Watahiniwa wa PSPTB waliomaliza mitihani ya kitaaluma ya Awali ngazi ya pili (Basic Stage II), mitihani ya kitaaluma ngazi ya Msingi (Foundation Stage I and II), Mitihani ya Kitaaluma ngazi ya kwanza, pili, tatu na nne (Professional Stages I, II, III and PIV) ndani ya miaka mitano kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala wa Kitaaluma.
- (e) Watahiniwa wote wanaorudia baadhi ya masomo katika ngazi mbali mbali ndani ya miaka mitatu kwa mujibu wa matakwa ya Mtaala mpya.

NB.

- (i) Watahiniwa wanaorudia mitihani zaidi ya ngazi moja wanaruhusiwa kuunganisha ngazi mbili zinazofuatana (Two Consecutive Levels) kwa masomo kuanzia mawili hadi sita tu, na kwa kuzingatia ratiba ya mitihani ya 2 ya PSPTB. Hivyo, waombaji wote wanashauriwa kuangalia ratiba ya mitihani kabla ya kuomba kufanya mitihani hiyo.
- (ii) Ada za mitihani tajwa zimewekwa kwenye tovuti ya PSPTB.
- (iii) Uendeshaji wa mitihani mingine inayofanyika Novemba na Mei itaendelea kama kawaida.

Kwa maelekezo au ufafanuzi zaidi tafadhali piga simu namba **0738441972** au tuma barua pepe kupitia **examinations@psptb.go.tz**

Imetolewa na :

GODFRED MBANYI
MKURUGENZI MTENDAJI